



THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

SCHOOL BASED ASSESSMENT

KISWAHILI

SEHEMU A

Zoezi la 2

Kusoma kwa Sauti

Gredi ya 4

NAKALA YA MWANAFUNZI

Pendo ni afisa wa afya. Juma lililopita alikuja shuleni mwetu. Alikuja kuzungumza kuhusu ugonjwa wa kipindupindu. Ugonjwa huu ulikuwa umeenea kijijini mwetu.

Afisa Pendo alituambia kuwa kipindupindu ni ugonjwa unaoenea kwa haraka. Alisema kwamba dalili za ugonjwa huo ni kuumwa na tumbo, kuendesha na kutapika. Alituhimiza kutafuta usaidizi endapo mmoja wetu angeonyesha dalili za kipindupindu.

Pendo alisema kuwa ni muhimu tuzingatie usafi. Tunawe mikono baada ya kutoka msalani. Alisema pia tunawe mikono kabla ya kula. Afisa Pendo alituhimiza tuchemshe maji ya kunywa. Alisema maji hayo yatiwe kwenye vyombo safi ili yawe salama.